



ATD Dunia ya Nne, Tanzania

Ripoti ya mwaka 2012





ATD Dunia ya Nne, Tanzania

Ripoti ya mwaka 2012

ATD Dunia ya Nne

(imesajiliwa kwa namba 003447 chini ya sheria ya Asasi zisizo za kiserikali ya mwaka 2002)

S.L.P. 61786, Dar es Salaam, Tanzania

Barua pepe : atd.tanzania@gmail.com

Tovuti ya Kiingereza : www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html

Tovuti ya Kiswahili : www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html

ATD Dunia ya Nne - Tanzania

Ripoti ya mwaka 2012

1. SEHEMU YA KWANZA - UTAMBULISHO WA ATD DUNIA YA NNE.....	5
1.1. Sisi ni nani?.....	5
1.1.1. Ni shirika la Kimataifa.....	5
1.1.2. Pamoja katika Utu.....	5
1.1.3. Muundo wa ATD Tanzania.....	6
1.2. Tunataka nini?.....	7
1.2.1. Kuushinda umaskini uliokithiri.....	7
1.2.2. Umaskini uliokithiri ni kitu gani?.....	7
1.2.3. Vipaumbele na miradi ya ATD Tanzania.....	8
1.3. Tunafanyaje kazi?.....	9
1.3.1. Kusikiliza kwa makini na kuelewa.....	9
1.3.2. Kuwa pamoja na kutafakari pamoja.....	9
1.3.3. Kutambua na kutafuta ufumbuzi.....	10
1.4. Tunafanya wapi kazi?.....	11
1.4.1. Tandale.....	11
1.4.2. Tegeta (Kunduchi na Boko).....	11
1.4.3. Soko la Samaki – Magogoni.....	11
2. SEHEMU YA 2: MAFANIKIO MUHIMU YA ATD DUNIA YA NNE - 2012.....	12
2.1. Kuwapa uwezo na majukumu.....	13
2.1.1. Shabani na Venance.....	13
2.1.2. Selemeni na Hassan.....	15
2.2. Kuimarisha shirika la ATD Tanzania.....	17
2.2.1. Kundi la washauri.....	17
2.2.2. Kundi la vijana marafiki.....	17
2.2.3. Warsha “Kufanya kazi pamoja kama washirika walio sawa”.....	18
2.2.4. Mchakato wa mukutano mkuu.....	19
2.2.5. Maadhimisho ya siku ya kuushinda umaskini ulio kithiri.....	20
2.2.6. Maktaba ya mtaa.....	21
2.2.7. Majarida.....	21
2.3. Watoto maskini kupata shule.....	22
2.3.1. Elimu ina umuhimu gani kwa ATD?.....	22
2.3.2. Kwa nini watoto wengine hawaendi shulen?.....	22
2.3.3. Jinsi ATD inavyosaidia watoto kupata shule.....	23
2.3.4. Watoto wangapi walikwenda shulen?.....	23
2.4. Watoto maskini sana wanapata vyeti vyao vya kuzaliwa?.....	24
2.4.1. Kupata vyeti vya kuzaliwa kuna maana gani kwa ATD?.....	24
2.4.2. Kwanini watoto hawana vyeti vya kuzaliwa?.....	24
2.4.3. Njia gani inatumwiwa na ATD kuwasaidia kupata vyeti vya kuzaliwa?.....	25
2.4.4. Watoto wangapi walipata vyeti?.....	25
2.5. Watu wazima maskini wanajifunza kusoma na kuandika.....	26
2.5.1. Nini maana ya kupata elimu kupitia ATD?.....	26
2.5.2. Kwa nini baadhi ya watu wazima hawajui kusoma na kuandika?.....	26
2.5.3. ATD inawasaidiaje kujua kusoma na kuandika?.....	26
2.5.4. Ni watu wangapi walijifunza kusoma na kuandika?.....	27
3. MWELEKEO KWA MWAKA 2013.....	28



Syo kwamba watu wanahitaji chakula kingi au nguo kwamba wanachohitaji ni utu na kutotegemea fadhila kutoka kwa wengine,

{“Joseph Wresinski mwanzilishi wa ATD}

Kama ilivyo ATD Dunia ya Nne Tanzania kutoa taarifa ya kila mwaka ni fursa kuelezea mabo muhimu yaliyo fanyika, pamoja na mafanikio, mambo tuliyo shiriki na kujifunza kuhusu mapambano ya kuushinda umaskini uliokithiri.

Chanzo cha taarifa hii ya mwaka 2012 ni kutoka kwa wale wanao husika na ATD Dunia ya Nne Tanzania, na tumaini letu ni kutokana na maelezo yao na ushuhuda wao utaielewa vema ATD Dunia ya Nne {Sehemu ya kwanza} na pia kujua ni shughuli gani muhimu tulizozifanya na mafanikio ya mwaka 2012 {Sehemu ya pili}

Hatutarudia tena kueleza malengo manane tuliyo changanua na rafiki zetu mwaka 2009. Malengo haya bado ni mwongozo wetu. Utayasoma katika taarifa ya mwaka 2009 ukurasa wa 15 na 16. Tovuti: www.atd-fourthworld.org/Annual-report-2009.html

Sehemu ya kwanza - Utambulisho wa ATD Dunia ya Nne.

1.1. Sisi ni nani?

1.1.1. Ni shirika la Kimataifa

ATD Dunia ya Nne ni shirika la Kimataifa lisilohusiana na dini wala siasa, lilianzishwa huko Ufaransa mwaka 1957. Kwa sasa lina wanachama wa kudumu katika nchi 32 duniani katika mabara matano katika nchi zilizoendelea na zisizoendelea, Tanzania ni nchi moja wapo..

Likiwa shirika la Kimataifa kwa muda wa miaka 50, limefanikiwa kupata ujuzi mkubwa wa kujifunza mambo mengi kutoka nchi nyingi zenyetamaduni tofauti, ujuzi huu hujadiliwa kwa kutumia njia tofauti, kama vile mikutano, taarifa na mitandao.



"Kila mara tunabahatika kusoma shuhuda kutoka nchi nyingine duniani, inasaidia sana kuujua umaskini uliokithiri. Nilikuwa sijui kama kuna umaskini uliokithiri duniani." - Rachel mwanafunzi wa ATD.

1.1.2. Pamoja katika Utu

Maneno haya ATD- "Pamoja katika utu" yanaelezea kwa kifupi sisi ni nani tunataka nini na jinsi tunavyo fanya kazi zetu. "Pamoja" inaeleweka, kwani linatufahamisha kuhusu umoja wa shirika, pia ulazima wa kushirikiana katika juhudzi za kila mmoja ili kufikia malengo..



"Kuwa pamoja ni mkusanyiko wa watu wanaofanya kitu fulani, kuchangia na kutoa mawazo. Hunifanya nijione kuwa na mimi ni binaadamu. Ni wakati wa kujifunza kutoka kwa wengine" - Selemani Yasini, muuza pweza, soko la samaki.



"Kuwa pamoja ni wakati wa kushirikiana kati ya majirani, rafiki au katika jamii, Inasaidia kuwafanya watu waishi kwa amani, wakisaidiana na kufahamiana" - Mohamed Shaa, mpaa samaki, soko la Samaki.

Fikra ya "Utu" inachanganya sana, lakini muhimu ni kama moyo wa ATD. Wanaharakati na marafiki hueleza kwamba "Utu" hupelekea kila mwanaadamu kuwa na thamani, pia kila mmoja anastahili kuhestimika. Utu ni asili ya binaadam, kwani kila mtu ana utu. Vile vile, katika hali fulani, binadamu hawaheshimiani.

"Binaadamu wote ni sawa. Hata ukiwa tajiri au maskini haki ni sawa kwa wote. Inakupa utu. maskini hawana haki kwa hiyo hujiona kama wamedhraulika. Anatakiwa mtu wa kuwatia moyo wasimame ili kuelewa kuwa wana hadhi na haki sawa na wengine." - Saasita, Mwanaharakati



"Kwangu mimi utu ni njia bora ya kufikia yale yanayo kufanya uishi kwa amani katika jamii. Popote pale maskini hawaheshimiwi. Jukumu la ATD ni kuwawezesha wale wasio thaminiwa wathaminiwe nao wajione kuwa wana thaminiwa". - Fredrick, mwalimu na mchungaji.

1.1.3. Muundo wa ATD Tanzania

Shirika lilianza kufanya kazi hapa ncini mwaka 1999 na lilisajiliwa kama Shirika lisilo la kiserikali mwaka 2009. Chini ya Sheria ya mashirika yasiyo ya kiserikali ya mwaka 2002. Namba yake ya usajili NGO/00003447. Ni sehemu ya Shirika la Kimataifa la ATD Dunia ya Nne.

ATD Tanzania siyo Shirika la utawala. Lina wanachama wa tabaka zote na vikundi vyenye majukumu mbalai mbali vyenye mshikamano thabiti.

Wanaharakati

Wanaharakati wanaishi katika umaskini uliokithiri. Wanao ujuzi wa kupambana na umaskini katika maisha yao ya kila siku pia wakiwasaidia wengine kuushinda umaskini. Wanajihuisha na miradi. Wengi wanaishi Dar lakini wengine wapo mikoani.

Rafiki

Rafiki ni watu ambao siyo lazima wawe wamekumbana na hali ya umaskini bali wamejenga uhusiano baina ya jumuia au kazi zao na watu wanaishi katika umaskini uliokithiri. Wengine wako kwenye vikundi vingine. Wanayo shauku ya kulisaidia shirika na kujitolea kushirikiana na watu maskini. (Wanaharakati, timu, kundi la rafiki vijana, kundi la washauri.)

Timu


Mwaka 2012 ATD Tanzania ilikuwa na wanaharakati 6 wa kudumu: Watanzania watatu na watatu kutoka nchi za nje. Watatu wapo kwenye kikosi cha wanaharakati wa kudumu wa kujitolea. Waliobaki walikuwa wanafunzi. Kundi hili linawasaidia wanaharakati na rafiki katika shughuli na miradi mbali mbali. Timu hii inahusika kuendesha na kusimamia shughuli za ofisini na kuwa na mawasiliano ya karibu na Makao Makuu ya ATD huko Ufaransa.

Kundi la washauri

Kundi dogo la rafiki na wanaharakati wamekuwa wakikutana mara kwa mara kuanzia mwezi Septemba mwaka 2008. Wanachama hawa ni mashahidi na washauri kuhusu maendeleo ya Shirika hapa nchini.

Kundi la vijana rafiki

Tangu Januari 2010 kundi la vijana rafiki wa ATD hukutana kutafakari majukumu ya vijana ya kuijenga dunia yenye haki. Wanatoka katika jamii tofauti katika maeneo ya Dar es Salaam.



1.2. Tunataka nini?

1.2.1. Kuushinda umaskini uliokithiri

Lengo kuu la Shirika la ATD ni kuushinda umaskini uliokithiri ili kujenga jamii sawa yenyewe kuthamini utu na haki za binadamu. ATD inalenga kumsaidia maskini na familia maskini kwa kuwepo kwake kuanzia ngazi za chini na kuhusisha jumuia zilizo maskini na kuziwezesha kuutambua umaskini uliokithiri na kuweka taratibu za kukabiliana nao.

"Madhumuni ya ATD ni kuondoa tofauti zilizopo kati ya tajiri na maskini. Idadi kubwa ya maskini kama sisi hufikiri kuwa dunia ni ya matajiri, la hasha, dunia hii ni yetu sote". - Shabani, mvunja mawe machimbo ya Boko.



1.2.2. Umaskini uliokithiri ni kitu gani?

Inaeleweka kwa ujumla kuwa umaskini uliokithiri ni kukosa mtaji. Hii ni kweli kwani fedha inawezesha kupata vitu vya msingi na huduma kama vile chakula, maji, makazi au usafiri. Umaskini uliokithiri una wigo mpana. Hauwezi kupunguzwa kwa muelekeo wake wa kiuchumi.

Wanaharakati na marafiki huelezea kuwa umaskini uliokithiri ni hali ambayo inakufanya kuwa tegemezi, unatengwa na jamii, ambapo haki za binadamu haziheshimiwi, ambapo huwezi kuelezea mbele za watu na pia hakuna tumaini la kuwa na hali nzuri hapo baadaye.

"Mtu anayeishi katika umaskini ni yule ambaye anayeshindwa kupata chakula, hana nyumba, kazi, elimu lakini cha msingi ni kwamba anahitaji msaada ili aishi" - Mama Niko, mama wa nyumbani.



*"Ukiwa kwenye mkutano wa familia mara nyingi maskini hapewi nafasi ya kuzungumza. Ukiwa maskini huna mchango katika jamii, unapokwenda hospitali au kwenye ofisi, hupewi heshima. Sio kitu cha aibu kuishi katika umaskini lakini umaskini ni aibu. Unashangaa kwanini siyo mtu muhimu kwani ni binadamu kama wengine." - Ally fundi umeme, mkulima na mjumbe wa nyumba 10 Kibaha.*

1.2.3. Vipaumbele na miradi ya ATD Tanzania

Mwaka 2010 ATD ilipanga kuwa na vipaumbele vinne. Vipaumbele hivi vinaliwezesha Shirika kupanga kushughuli zake na miradi. Ni vema kuelewa vizuri ATD inataka kufanikisha nini hapa Tanzania?

- Kuwasaidia wanachama kuhusu maendeleo ya Shorika hapa Tanzania.**

Maendeleo ya ATD na kuwawezesha wanachama (wanaharakati na marafiki) ni jambo muhimu kwani wanapaswa kuwa viongozi wa shughuli hapa Tanzania. Tutaona katika sehemu ya pili ya taarifa hii kuwa jambo hilo lilikuwa na mafanikio mwaka 2012.

- Kuwasaidia kupitia shughuli na miradi wale wasio bahatika kuhusu changamoto wanazo kabiliana nazo.**

Wanachama wa ATD wanachukua hatua madhubuti kuwasaidia maskini. Mwaka 2012 kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, ATD ilitekeleza miradi inayolenga kufikia haki za msingi: elimu kwa watoto, vyeti vya kuzaliwa na elimu ya watu wazima. Katika sehemu ya pili tuitaelezea mafanikio.

- Kuanzisha uhusiano wa karibu na kanda na dunia**

Likiwa ni Shirika la Kimataifa, ATD linamawasiliano ya karibu na timu kutoka nchi mbali mbali. Linawasaaidia wanaharakati na rafiki kufahamu haki kuhusu umaskini ulivyo katika nchi nyingine. Inawawezesha kutambua kuwa majukumu yao ni sehemu kubwa katika kupambana na umaskini ulio kithiri.

- Kuimarisha haki yetu kifedha na utawala.**

ATD inawajibika vizuri katika kudhibiti mambo ya utawala na fedha. Lina maadili imara ya kuijidesha. Kuhakikisha kuwa fedha hazitumiwi vibaya kwa shughuli zisizokuwa za maana. Ni jambo muhimu kwa ATD kuijidesha na pia kutekeleza mradi. Taarifa ya fedha inaelezwa kwenye kiambatanisho.



1.3. Tunafanyaje kazi?

Shirika la ATD linawasaidia watu wanaoishi katika umaskini ulio kithiri kupata haki zao na kujenga uhusiano na watu na taasisi tofauti: Watu wanaoishi katika umaskini ulio kithiri ndio kiini cha shirika. Ndiyo maana wanashiriki katika muafaka wa kuushinda umaskini ulio kithiri.

1.3.1. Kusikiliza kwa makini na kuelewa

Wanachama wa ATD binafsi husikiliza watu wanaoishi katika umaskini ulio kithiri. Jambo hili ni muhimu kwani mara nydingi vilio vyao havisikiki, hata kama ni wao wanaolewa ugumu wa hali yao. Hii ni sehemu ya utu; watu wote wana kitu cha kusema na wanayo haki ya kusikilizwa.

"Ninapenda jinsi ATD inavyowasikiliza watu. Endapo tutakwenda kukutana na matajiri na wasomi wasinge tueleza chochote kwa kuwa tu maskini na kwamba wangelidhania kuwa hatutaelewa" - Mama Msham, mama wa nyumbani Tandale.



"ATD inawasikiliza watu na kushauriana Njia hii inawezesha kugundua tatizo kisha kufikia muafaka." - Mama Athumani- mpishi Tandale.

1.3.2. Kuwa pamoja na kutafakari pamoja

ATD inawakutanisha maskini na wasio maskini ili wafahamiane watafakari hali zao, wabadilishane ushuhuda ili kuelewa kiini cha umaskini .*Umuhimu wa kufanya hivi ni kwamba wanagundua kuwa siyo peke yao wanaokumbana na tatizo hili, kwamba umaskini siyo jambo la asili kwamba wana haki na watu wanajali haki waliyo nayo. Kuwa pamoja kunawapa imani na tumaini*

"ATD ni kama chama ambacho watu hukutana na kushirikiana kuchangia mawazo juu ya hali zao.Kama kuna tatizo unaweza kupata ushauri kutoka kwa wengine ambaa hali zao zinafanana na yako." - Baba Godfrey, mlinzi na fundi miamvuli Tandale.



"ATD ni mahali ambapo maskini na maskini sana hukutana kufanya shughuli pamoja na kubadilishana mawazo kuhusu hali yao badala ya fedha. Ukitoa pesa kwa wale wanaokuja kwenye mkutano ni kwamba watakuja kwa ajili ya kupata fedha. Mimi nikirudi nyumbani ninaweza kueleza niliojifunza." - Mama Mshamu, mama wa nyumbani Tandale.



"Zamani nilikuwa siwezi kuzungumza mbele ya watu wengi. Sasa naweza kuongea mbele ya watu zaidi ya 200.Nilikuwa naogopa kuchekwa. Mfano ni kwamba sikuweza kusema kitu kwenye mkutano wangu wa kwanza wa ATD. Sasa nimebadilika" - Mohamedi Selemani- Mpaa samaki

1.3.3. Kutambua na kutafuta ufumbuzi

Hakuna njia maalumu iliyo rahisi ya ufumbuzi wa jinsi ya kuushinda umaskini uliokithiri. Hii inatokana na kuwa na mifumo yenyeye dhuluma katika nyanja za siasa, jamii, uchumi na utamaduni. Kwahiylo kila hali iko tofauti na wakati mwingine ngumu. Lakini ufumbuzi upo. Kuwa pamoja kunawafanya kuwa imara. Hata hivyo wanatambua kuwa wanazo haki na kwamba wanaweza kuzipigania. Pamoja na kuelewa na kupata ushauri kutoka ATD wanalenga kufikia kupata ufumbuzi wa kudumu kuhusu maswala yao.



"Kabla ya kuwa na ATD tulidhani kuwa mambo mengi yalikuwa hayawezekani kwa mfano mtoto kupata uhamisho wa shule. Sasa tunajua kwamba kila kitu kinawezekana" - Mama Sele wa Tegeta.

"Nilitambua kuwa maisha ninayoishi hayakuwa ya kawaida. Nilitambua kuwa umaskini uliokithiri siyo jambo la kawaida. Jukumu la ATD ni kuwaelimisha watu kuhusu umaskini ulio kithiri. Nashukuru ATD kwa kunielimisha. Niko tayari kuamini kuwa siku moja umaskini ulio kithiri utatokomezwa" - Bi Agnes mvunja mawe machimbo ya kokoto Kunduchi.



"ATD ilinisaidia kugundua na kujitambua kuhusu hali yangu ya umaskini. ATD inatusaidia kuelewa kuwa umoja ni nguvu." - Kasian wa machimbo Kunduchi.



1.4. Tunafanya wapi kazi?

Hapa Tanzania ATD imejikita kufanya kazi katika maeneo matatu ya jiji la Dar es Salaam; huko Tandale, Tegeta (Kunduchi na Boko) na soko la samaki Magogoni. Kwa zaidi ya miaka 10 ATD imeanzisha uhusiano na watu wengi na familia zinazo ishi katika maeneo hayo.

1.4.1. Tandale

Nikitongoji cha Dar es Salaam kilicho kati kati ya Sinza na Manzese. Watu wanao ishi pale ni watu wa tabaka mbali mbali. Sehemu nyingine zina hali ya umaskini na zimechakaa. Kwa muda wa miaka 10 ATD imewezesha miradi mbali mbali na kuanzisha uhusuano na watu pamoja na familia zaidi ya 100.



1.4.2. Tegeta (Kunduchi na Boko)

Tegeta ni kitovongoji kilichopo maili kama 20 kaskazini ya Dar es Salaam. Kipo karibu na maeneo ya machimbo ya kokoto kama vile Kunduchi na Boko mahali ambapo watu zaidi ya elfu moja wanafanya kazi ya kuvunja mawe au wanapakia kokoto kwenye magari. Wavunja mawe siyo wa jinsia moja, wazee na vijana na hata watoto. Wengi wao ni maskini sana. Ingawa wengi wanaamini kuwa ipo siku wataondoka, lakini hukaa pale kwa miaka mingi.

1.4.3. Soko la Samaki – Magogoni

Soko la Samaki Magogoni ni kubwa sana hapa Dar es Salaam. Zaidi a watu 300 hufana kazi hapa. Wanafanya kazi na biashara za kila aina kama vile kuuza mboga, vyakula, mkaa na kuni, barafu kupaa na kukaanga samaki n.k. Wengi wao ni maskini ambao kila siku wanatafuta shughuli ndogo ndogo ili wapate riziki. Kuna vyama 15 vinavyowakilisha makundi haya.



Sehemu ya 2: Mafanikio muhimu ya ATD Dunia ya Nne - 2012

Mwaka 2012 ATD Dunia ya Nne Tanzania ilifikia hatua mpya katika mapambano dhidi ya umaskini uliokithiri na kutekeleza haki za binadam. Mafanikio hayo yalifikasiwa kwa kuwapa uwezo na kujitolea zaidi kwa wanaharakati wa ATD Tanzania (Fanikio la 1) na kuimarisha ATD Tanzania (Fanikio la 2). Kwa juhudui kubwa wanachama wa ATD waliwasaidia watu na familia maskini kupata shule (Fanikio la 3) kupata vyeti vya kuzaliwa (Fanikio la 4) na kujifunza kusoma na kuandika Kiswahili(Fanikio la 5).

Mafanikio mawili ya kwanza ya ATD yana maana sana kwani watu waliweza kuchukua hatua siyo kwa ajili yao tu bali kwa ajili ya jumuia zao pia ili kuushinda umaskini uliokithiri. Uhusiano mzuri na marafiki kutoka serikali za mitaa, wakuu wa shule na ofisi ya msajili wa vifo na vizazi.ATD inaamini kuwa njia hii ni sahihi ili kuushinda umaskini ulio kithiri na kuifuata kuwa ni njia sahihi ya kudumu kwani inawapa nguvu, uwezo na madaraka na kuchukua hatua kwa ajili ya maisha bora hapo baadaye.

Mafanikio 3,4,5 pia ni muhimu kwani kwa walio maskini sana walipata haki zao.Elimu na vyeti vya kuzaliwa ni muhimu katika hatua ya kuushinda umaskini ulio kithiri: Mafanikio haya yalifikasiwa na watu wenyewe kwa ushirikiano na timu ya ATD, rafiki na wanaharakati.



2.1. Kuwapa uwezo na majukumu

Watu wa kwanza kujenga ATD Dunia ya Nne ni wale wanaoishi katika umaskini ulio kithiri. Moja ya mafanikio mwaka 2012 yalikuwa ni kuwapa uwezo wanaharakati. Wengi wao wamejitolea sana kuwawezesha na kuwasaidia wengine kupambana na umaskini ulio kithiri. Siyo rahisi kuyaeleza yote katika ripoti hii: Yafuatayo ni maelezo ya wanaharakati wanne ambao kazi zao zilikuwa bora zaidi.

2.1.1. Shabani na Venance

Ni nani hao?

Shabani na Venance wanafanya kazi ya kuvunja mawe huko machimbo ya Kunduchi na Boko. Ni wanaharakati wa ATD pia wanahuksika na kundi la washauri licha. Licha kukabiliwa na changamoto ya kutekeleza majukumu kwenye familia zao, hupata muda wa kusadia jumuia zao. Hujitolea.



"Jina langu ni Shabani na nilizaliwa hapa Tegeta, niliishi na baba yangu hadi nilipooa. Nina elimu ya msingi ya darasa la 7. Baba alinipeleka machimbo kufanya kazi. Ninao watoto watatu. Maisha yangu ni magumu. Ninajitahidi kuwalea wanangu licha ya kwamba sina fedha. Pia ninajitahidi kutenda mema katika jumuiya yetu. Elimu ni kitu muhimu hivyo nina hakikisha wanangu wanaenda shulen kila siku".



"Ninaitwa Venance na nilikulia Morogoro. Nilikuja Dar es Salaam nilipokuwa na umri wa miaka 19. Nimesoma shule ya sekondari ya Azania mpaka kidato cha nne. Nimeoa na nina watoto watano. Nilianza kufanya kazi ya kuvunja mawe miaka 20 iliyopita hapa Kunduchi."

Mwaka 2012 Shabani na Venance walishiriki kikamilifu vikao vya kundi la washauri: walisaidia timu ya ATD katika maandalizi na kuwezesha warsha na mikutano: waliandaa sherehe ya siku ya Kimataifa ya kuushinda umaskini ulio kithiri, waliwatembelea rafiki wa ATD kule Njombe , walisaididua na kutoa ushauri wa jinsi ya kuyakabili matatizo magumu kwenye jumuiya zao kama vile kupata shule na vyeti vya kuzaliwa. Katika kifungu kifuatacho tutaangalia juhudzi zao katika mradi wa vyeti vya kuzaliwa.

Mfano wa juhudzi zao: Mradi wa vyeti vya kuzaliwa

Mwaka 2012 Shabani na Venance walihusika na mradi wa vyeti vya kuzaliwa huko Kunduchi na Boko. Inawachukua muda wa siku kadhaa katika mwezi kuzifikia familia maskini katika sehemu za kazi zao na wanapoishi kuwaelimisha jinsi ya kuandaa taarifa na kujaza fomu (maelezo, nakala za vielelezo na picha) kuwapeleka RITA na kugawa vyeti. Wanafanya kazi pamoja wakisaidiana majukumu na kuhamasishana.



"Zamani nilikuwa sijui utaratibu wa kusajili vizazi. Kwa msaada wa ATD nilikwenda kwenye ofisi za RITA kuwasajili wanangu wanne hapo ndipo nilipozilelewa taratibu za kusajili. Pia nilihudhuria mikutano mingi ya ATD. Ndipo nilianza kuelewa zaidi" - Venance.

Wameonyesha uwezo mkubwa katika utendaji wao na wanafamilia kusajili watoto wengi. Wanajuhudi kwa kuwa nao wanaishi katika maeneo hayo wanawajua watu nao wanafahamika. Kwa hiyo ni rahisi kwao kuwatambua maskini sana na watu wanaohitaji vyeti vya kuzaliwa, kuwasiliana kwa njia sahihi na kujenga uaminifu na kuwashauri kufuata utaratibu.

Shabani na Venance wameamua kujipanga vizuri. Wameanza kuweka kumbukumbu zote zinazohusu utaratibu ili kurahisisha ufuutiliaji.



Kwanini wamechukua jukumu?

Shabani na Venance hawalipwi fedha na wala hawapewi vitendea kazi. Si kitu cha kawaida hapa Tanzania kwani katika taasisi nyingi, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za Kimataifa watu hulipwa kwa kuhudhuria mikutano na vikao - "Posho ya kikao." Utaratibu huu huanzisha tabia ya kuwa tegemezi ambapo majukumu hutegemea zaidi fedha kuliko kupenda kwa utashi. Matokeo yake ni kutokea mashaka wakati watu kama Shabani na Venance wanaposimamia haki zao na kujitolea kwenye jumuiya zao. Sababu zao ni za kawaida na za msingi.



"Inanisaidia kupata changamoto. Ninajua nafasi yangu katika jamii na ninajua nifaye nini kwenye jumuiya yangu. Pia ni njia ya kupata ujuzi mpya. Lazima tuwajali wale wanaishi katika umaskini, tusiwatenge." - Shabani.



Ninataka kuwasaidia wangine kwasababu mimi pia nilisaidiwa. Nilipokea nami nataka kutoa. Kwangu mimi tajiri na maskini wote ni binadamu. Tusijenge tabaka kati yao." - Venance.

2.1.2. Selemeni na Hassan

Ni nani hao?

Selemeni na Hassan wanafanya kazi soko la samaki Magogoni: Ni wanaharakati wa ATD na wajumbe wa kundi la washauri. Huko soko la samaki Selemeni na Hassan ni watu wa kukumbukwa na pia ni alama nzuri ya kuwafikia maskini sana. Wana julikana na pia ni kiungo muhimu kwa mawasiliano na wale walio maskini sana.



"Jina langu ni Selemeni, kila siku ninaamka mapema kuja hapa soko la samaki Magogoni. Ninaishi Mbagala. Ninauza pweza kwa hakika ninafanya kazi katika mazingira magumu sana."



"Ninaitwa Hassan ninatoka kitongoji kilicho kusini mwa Dar es Salaam. Nilikuwa nafanya kazi ya kupakia samaki kwenye meli iliyokuwa inafanya safari za kwenda Mafia na Zanzibar. Lakini mwaka 2005 kampuni ilifungwa. Nilikuja hapa soko la samaki kutafuta kazi."

Mwaka 2012 waliweza kuandaa na kushiriki katika shughuli nyingi na matukio. Kwa mfano walihusika pamoja na timu ya ATD kuandaa maadhimisho ya tarehe 17 Oktoba hapo soko la samaki. Pia walishiriki kikamilifu kwenye warsha ya "Kufanya kazi pamojakama washirika" na mchakato wa mkutano mkuu. Katika kifungu kifuatacho tutalenga na kuangalia juhudhi zao za kuendesha darasa la elimu kwa watu wazima hapo soko la samaki.


Mfano wa kuhusika kwao: darasa la watu wazima

Mwaka 2010 na 2011 ATD ilianzisha darasa kusoma kwa watu wazima, ambapo Hassan na Selemen walishiriki kama wanafunzi. Hata hivyo kukosekana kwa ari, kutoka kwa wanafunzi, ATD iliamua kusitisha masomo hapo soko la samaki.

Hassan na Selemeni walikaia tamaa kwa uamuzi huo. Kwao darasa liliikuwa kitu cha muhimu zaidi. Waliona kuwa lingekuwa na faida kwa watu wengine. Walianza kuzungumzia mradi huu na wenzao hapo soko la samaki. Waligunda kuwa wengi walikuwa na shauku ya kujifunza kusoma na kuandika.



"Huwa nawaambia rafiki zangu ATD ni kitu gani na pia ninajaribu kuwashawishi wajunge na darasa la kisomo cha watu wazima. Nawaeleza kuwa nilikuwa sijui kusoma na kuandika kisha wanagundua kuwa imewezeekana na bila shaka itawezekana kwao pia." Hassan.



Walikuwa na imani kuwa wanaweza kupata wanafunzi. Waliwaomba ATD kuwasaidia kuanzisha darasa jipya. Mwezi Januari 2013 kutohakana na juhudhi zao darasa lilianza likiwa na wanafunzi 10. Hassan na Selemeni waliwasaidia wanafunzi wapya wakiwapa mbinu na mwelekeo wa kisomo hicho.

Kwanini walijihuisha?

Kama ilivyo kwa wanaharakati na marafiki wa ATD kuhusika kwao na shirika ni kitu walichokizoea. Ingawa maisha yao ni magumu wanaamini kuwa ni muhimu kuleta mabadiliko kwa maskini katika jumuiya zao.



"Kuhusika kwangu kunatoka moyoni kwangu. ATD ilinisaidia kujua kusoma na kuandika. Ilinigusa na sasa ninaweza kuwasaidia wengine. Ninataka wajue kusoma na kuandika. Nikiwa kwenye shughuli za ATD, rafiki zangu huko soko la samaki hunisaidia kufanya kazi zangu. Kazi yangu na maisha ni magumu, wakati mwininge huwa sina hata fedha" - Hassan.



"Ni muhimu kwangu kuhudhuria mikutano na kushiriki katika shughuli za ATD kwa kuwa ninaweza kutoa maoni kuhusu masuala mbali mbali. Ujumbe wangu unasikika katika jamii na unaweza kuleta mabadiliko." - Selemani.



2.2. Kuimarisha shirika la ATD Tanzania..

Mwaka 2012 fanikio muhimu la pili lilihusika na kuimarisha ATD hapa Tanzania. Mipango ya uimarishaji ilianza zamani nayo itakuwa endelevu. Hata hivyo tunafikiri kuwa mwaka 2012 ulikuwa muhimu kwa maendeleo ya shirika.

Mwaka uliopita wanachama walikutana mara kwa mara, walijenga mshikamano imara na washirika, walibadilishana taarifa, walijihuisha na shughuli na walidumisha uhusiano wao na shirika la Kimataifa la ATD Dunia ya Nne.

Katika sura hii tutaeleza kwa ufupi vyanzo viliivo wezesha kuimarika kwa shirika. Kundi la washauri, kundi la vijana marafiki, Warsha (“Kufanya kazi pamoja kama washirika walio sawa”), mchakato wa Mkutano Mkuu, maadhimisho ya siku ya kuushinda umaskini ulio kithiri duniani, maktaba ya mtaa na majarida.

2.2.1. Kundi la washauri



Kila wakati wa mkutano mwaka 2012, Kundi la washauri lilipata taarifa sahihi kuhusu shughuli za ATD kitaifa na kimataifa. Pia kundi la washauri lilihiriki katika mchakato wa mkutano mkuu warsha, “kufanya kazi pamoja kama washirika walio sawa” madhimisho ya siku ya kuushinda umaskini ulio kithiri duniani na shughuli za ATD za kufanya tathmini.

Mwezi Novemba 2012 hatua muhimu ilichukuliwa na kundi la washauri. Ilikubaliwa kuwa kundi hili lionegeze wajumbe na hivyo walionegeza saba. Wanaharakati kutoka Kunduchi, Soko la samaki Magogoni na Tandale. Hatua hii ilisaidia kuleta mawazo mapya na kuweka uwiano kati ya wanaharakati na wajumbe marafiki.

2.2.2. Kundi la vijana marafiki

Mwaka 2012 kundi la vijana marafiki walikutana mara kumi na moja. Mwanzoni mwa mwaka walianzisha kanuni za kundi, walijadili masuala mbali mbali kama vile mwongozo wa ATD Dunia ya Nne au njia mahususi za kuwafikia watu maskini sana. Wengine walishiriki warsha kuhusu mada ya “Kufanya kazi pamoja kama washirika walio sawa” mchakato wa mkutano mkuu na maadhimisho ya Siku ya Kuushinda Umaskini ulio kithiri.



2.2.3. Warsha “Kufanya kazi pamoja kama washirika walio sawa”

Tarehe 20 na 21 Aprili ATD waliandaa warsha mada ikiwa “Kufanya kazi pamoja kama washirika walio sawa.” Lengo la warsha hii lilikuwa ni kuanzisha uhusiano kati ya maskini sana na wataalam wanaofanya kazi katika taasisi mbali mbali kama vile shule, hospitali, RITA au serikali za mitaa.



Kulikuwa na washiriki zaidi ya sitini pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kimataifa la ATD Dunia ya Nne na wajumbe wawili wa ATD Dunia ya Nne Kanda ya Afrika. Mipango ilifanywa ili kumwezesha kila mmoja kuzungumza hasa wale ambao hawakuzoea kuongea mbele ya watu.

Washiriki walibadilishana mawazo kuhusu masuala mbali mbali kama vile tofauti iliyopo ya uhusiano kati ya makundi haya mawili, tabia, ubaguzi na uonevu uliopo na vikwazo wanavyokabiliana navyo wanapokutana. Mwishoni washiriki waligundua kuwa inawezekana kufanya kazi pamoja kama washirika na pia utu na kuaminiana kuwepo wakati wa kutoa huduma au kutekeleza majukumu au miradi.

“Tuangalie pande zote mbili bila ya kulaumiana. Tujaribu kuelewa ni kwa sababu gani watu wengine wanashindwa kujibu maswali yetu.” - Mjumbe wa serikali ya mtaa.

“Nimewapa taarifa wanayo ihitaji bila ya kuwafanya wajiskie vibaya.” - Mwalimu.

2.2.4. Mchakato wa mkuu

Mwaka 2012 ATD Dunia ya Nne iliingia kwenye mchakato wa Mkutano Mkuu na mashirika yaliambiwa kitaifa kujadili maana ya "Umoja katika mapambano dhidi ya umaskini ulio kithiri. Lengo la mchakato huu halikuwa ni kufikia muafaka baina ya wajumbe bali kuchangia mawazo, kujadili msimamo wa shirika na kujifunza mbinu mpya. Mkutano mkuu unachukuliwa kama utaratibu wa kufahamu kwa wanachama wote wa ATD.



ATD Tanzania ilianza mchakato huu kwa ushirikiano zaidi. Mwezi Juni, Agosti na Septemba mikutano kadhaa ilifanyika baina kundi la washauri, kundi la vijana marafiki, timu ya ATD, wanaharakati na marafiki wa shirika. Kwenye mikutano hii, wanachama wa ATD walishiriki na kujifunza mengi kuhusu maana ya "Umoja" kama Watanzania walio ndani ya shirika.

Mwezi Oktoba Mbaraka mjumbe wa kundi la washauri alikwenda Ufaransa ambako aliwakilisha mawazo yaliyo jadiliwa Tanzania.

"Tunafurahi zaidi tukiwa na wengine. Tunapata kujiamini na kuwa wazi: Kuwa na wengine kunatupa ujasiri wa kukabiliana na changamoto na kujua haki zetu. Tunapata nguvu kama kundi. Usijitenge kwani kushirikiana na wengine hukufanya ujisikie binadamu."



2.2.5. Maadhimisho ya siku ya kuushinda umaskini ulio kithiri

Oktoba tarehe 17 ni siku ya kuushinda umaskini Duniani. Siku hii iliadhimishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1987 na Shirika la ATD Ufaransa. Mwaka 1992 siku hii ilitambuliwa rasmi na Baraza la Umoja wa Mataifa.

Lengo la siku hii ni kuifanya jamii isikie kilio cha wale wanao ishi katika umaskini ulio kithiri, pamoja na kuyashawishi makundi yote ya jamii kutafuta njia za kutokomeza umaskini ulio kithiri na kutetea haki za binadamu.



"Ni siku muhimu sana. Kuzungumzia kuhusu umaskini uliokithiri. Ni fursa ya watu kuwa pamoja kutoa ushuhuda mbele ya washiriki kuhusu haki zao. Tunajaribu kuyafikia maeneo mengi hapa Tanzania, nchi mbali mbali na mabara tofauti." - Mbaraka mwakilishi wa wafanya kazi soko la samaki.



Mwaka 2012 ATD Tanzania ilibadilisha namna ya kuandaa kushiriki maadhimisho haya. Badala ya kuwa na sehemu moja ya kufanya, mwaka huu yalifanywa katika vikundi vidogo. Wanaharakati wa ATD walichukua jukumu la kuandaa na kuendesha maadhimisho haya katika sehemu zao za kazi, au mahali wanapoishi. Maadhimisho haya yalifanyika huko Tegeta, Manzese(Uwaba), Mbagala, Kibaha, Njombe, Dodoma na Magogoni.



"Jirani zangu waliguswa kuona kuwa maskini wana siku yao ya kuchangia mawazo yao pamoja na jamii nzima. Tukio linalo kuwezesha kugundua kuwa unaweza kujifunza kwa kuwasikiliza wengine." Ally fundi umeme, mkulima na mijumbe wa nyumba 10 Kibaha.



2.2.6. Maktaba ya mtaa

Maktaba ya mtaa ni shughuli muhimu ya ATD. Imekuwa ikitekelezwa kwa kipindi cha muda wa miaka kumi hapa Tanzania. Kila juma kuanzia mwaka 2003 wanachama wa ATD hupeleka vitabu, karatasi na pensili kwenye jumuiya maskini na kuanzisha "maktaba ya mtaa." Hukaa maeneo kando kando na kuwakaribisha watoto kusoma vitabu, kusikiliza hadithi, kuandika na kuchora. Hii inawapa watoto fursa ya kuelewa na kubadilishana mawazo. Kupitia maktaba ya mtaa wanachama wa ATD hujenga uhusiano na familia na kufahamu masuala yanayo zikabili jumuiya.



Kuanzia mwaka 2012 kila Jumatano ATD inaandaa maktaba ya mtaa huko Tandale. Wastani wa watoto .thelethini wenyе umri wa kati ya miaka 4 hadi 10 wamekuwa wakishiriki shughuli hii. Kwakuwa watoto wengi hawana vitabu nyumbani kwao. Maktaba ya mtaa ni sehemu yao ya kusikiliza hadithi. Pia ATD inawawezesha watoto kufikiri na kuzungumzia masuala muhimu yanayo jitokeza kwenye hadithi.

"Maktaba ya mtaa imebadilisha mambo mengi kwani kila Jumatano watoto hukutana na kufanya shughuli badala ya kuzurura au kuangalia picha za video. Wanaweza kubadilishana mawazo na watoto wengine." - Mwanaidi, mwanafunzi wa shule ya sekondari, Tandale.



2.2.7. Majarida

Kila baada ya miezi miwili, ATD hutuma majarida kwa watu 480 hapa Tanzania. Walengwa ni watu wanaoishi katika umaskini ulio kithiri, watumishi wa serikali, viongozi wa dini na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali. Mara nyingi walio maskini sana hupelekewa kwa mkono na wanachama wa ATD huwasomea au hukutana na kusoma pamoja.

Lengo la majarida ni kuwaunganisha watu binafsi na taasisi zilizo na jukumu la kupambana na umaskini ulio kithiri, kubadilishana shuhuda na kueleweshana kuhusu haki ya maisha ili kufanya wale wanaoishi katika umaskini ulio kithiri wajione kuwa hawatengwi na kuruhusu sauti ya maskini isikike ili kuonyesha kuwa wao ndio wapambanaji wa kwanza katika mapambano dhidi ya umaskini ulio kithiri.

2.3. Watoto maskini kupata shule

2.3.1. Elimu ina umuhimu gani kwa ATD?

Kupata elimu ni haki ya msingi ya binaadamu, pia ni njia sahihi inayosaidia kuushinda umaskini. Inawapa ufahamu, ujuzi na uwezo wa kuelewa mwelekeo wa maisha, kujumuika na watu wa kila tabaka, kujiamini, kupata ajira n.k.

"Watoto wanakwenda shule kwa msaada wa mradi huu amba ni hatua ya kwanza kuelekea kuufuta umaskini." - Mama Niko, mama wa nyumbani, Tandale.



2.3.2. Kwa nini watoto wengine hawaendi shulen?

Hapa Tanzania elimu ya msingi kwa maneno ni lazima nayo hutolewa bure. Lakini kutokana na utafiti uliofanywa, asilimia 21 ya wavulana wa 18 miaka na wasichana hawasomi.

Familia zilizo maskini sana zinashindwa kuwapeleka watoto wao shulen. Wanaharakati wa ATD wanasema kuna sababu zinazotofautiana. Familia maskini wanashindwa kununua sare za shule, vifaa, gharama nyingine na hongo. Watoto kukosa vyeti vya kuzaliwa. Baadhi ya wazazi kutokuelewa faida ya elimu, au watu maskini sana wanaweza kuwa hawana uwezo wa kuzifikia haki zao.



"Watoto wetu wanataka kwenda shule kusoma na serikali inasema kuwa elimu inatolewa bure lakini maskini hawana fedha za kununua sare za shule, daftari na hata kalamu." - Mama Asha, mama wa nyumbani Tandale.



"Wale wanao weza kujieleza na kuzijua haki zao wanaweza kwenda shulen kudai watoto wao wasome hata kama hawna vyeti vya kuzaliwa. Mtu maskini hawezi kufanya hivyo" - Happy mfanya kazi ya jamii.

2.3.3. Jinsi ATD inavyosaidia watoto kupata shule

Kupitia mradi wake "Kupata shule" wanachama wa ATD husaidia familia maskini kutambua ugumu wanao upata kuandikisha watoto wao shulen. Vikwazo hivi vikieleweka ATD inasaidia familia kutafuta njia za kuchukua ili kufanikisha watoto kwenda shulen.

Mara nyingi kufuatana na wazazi kwenda kukutana na mkuu wa shule au mkurugenzi inatosha kutatua tatizo. Wakati mwingine ATD husaidia kwa kutoa fedha kidogo kwa familia maskini inaposhindwa kutoa michango. Lakini sio kawaida kwa ATD kutoa msaada wa fedha, vile vile husaidia familia kupata vyeti nya kuzaliwa watoto wao. Misaada hii siyo suluhisho la muda mrefu, lakini linasaidia watoto kupata haki zao.

2.3.4. Watoto wangapi walikwenda shulen?

Mwaka 2012 wanachama wa ATD waliwezesha watoto maskini zaidi ya 50 kupata shule. Watoto hao wanatoka katika maeneo ambako ATD inafanya miradi yake.



2.4. Watoto maskini sana wanapata yeti vyao vya kuzaliwa?

2.4.1. Kupata yeti vyao vya kuzaliwa kuna maana gani kwa ATD?

Cheti cha kuzaliwa ni kitambulisho halali cha uraia wa mwananchi na kinatambuliwa na serikali. Ni hati muhimu kwani inampa mhusika fursa na haki zote za kupata elimu, ajira n.k. Kuwasaidia maskini kupata yeti vyao vya kuzaliwa, kazi inayofanywa na wanachama wa ATD ni hatua muhimu katika mapambano ya kuushinda umaskini ulio kithiri.

"Ukitaka kuwapeleka watoto wako shulenii inakuwa vigumu kwani huna cheti cha kuzaliwa cha mtoto. Elimu ni mwanga wa maisha yako kwani itakuwezesha kujua utafanya nini kuhusu maisha yako ya baadaye." - Mama Msham, mama wa nyumbani Tandale.



"Tuligundua kuwa kutowatafutia watoto wetu yeti vyao vya kuzaliwa tunawaweka katika hali ngumu katika maisha yao hapo baadaye." Wazazi wengine hawajui wajibu wao hivyo ni vyema tukachukua majukumu, siyo kwa watoto wetu tuu bali hata wale wa jirani zetu." - Wazazi wa Tandale.

2.4.2. Kwanini watoto hawana yeti vyao vya kuzaliwa?

Utaratibu ni kwamba unapata cheti cha kuzaliwa mtoto baada ya miezi mitatu tangu azaliwe. Hata hivyo watoto wengi wa maskini hawajasajiliwa. Usajili unatofautiana kulingana na umri na nyaraka zinazotakiwa (tangazo la uzazi, ganda la kliniki n.k.).



Hapa Tanzania ni asilimia ndogo sana ya watoto wenyewe umri wa miaka 0-5 wanavyo vyeti. Maskini wnanapata shida sana kuvipata. Wanachama wa ATD wanaelekeza sababu kuwa ni ukosefu wa fedha wa kulipia gharama, kukosekana kwa nyaraka zinazo hitajika na kutokuwa na uwezo wa kwenda ofisi za msajili. Wakati mwingine utaratibu huwa mgumu unahitaji nguvu za ziada na fedha..

"Utaratibu ni mgumu na watu wengi hushindwa, haswa maskini kwani wanakumbana na vikwazo na mara nyingi hukata tamaa. Watu kama hawa ndio wanasaidiwa na ATD, wale wanaogopa kwenda ofisini, wanaosema "namjua mtu fulani aliyenyanyswa, hivyo kwangu itakuwa vibaya sana"- Reachel – Mwanafunzi wa ATD.



"Wengi hatuna vyeti vyaa kuzaliwa vya watoto wetu. Tunajua kuwa siyo jambo zuri hapo baadaye, lakini hatujatafuta kutokana na sababu nyingi, ukosefu wa fedha, kukosa nyaraka, kukosekana kwa maelezo kuhusu utaratibu, mbali n.k." - Beatus mvunja mawe wa machimbo ya Kunduchi.



2.4.3. Njia gani inatumiwa na ATD kuwasaidia kupata vyeti vya kuzaliwa?

Kama ilivyoelezwa awali ATD hufanya mawasiliano na familia maskini kuwawezesha kuelewa umuhimu wa kuwa na cheti cha kuzaliwa na kuwatia moyo wakati wa taratibu za kusajili. Pia ATD hutoa msaada wa fedha, ikiziomba familia zote kutoa kima kimoja cha mchango bila kujali idadi ya watoto.



"Nadhani kuitia mradi huu wa kusajili vizazi tunapambana dhidi ya umaskini uliokithiri kwa kuwaelimisha wazazi tunapokutana nao, tunaweza kubadilishananao mawazo na kuwafanya wabadilishe matarajio yao, siyo kwa kukaa nyumbani na kusubiri, ndipo wanapoju jinsi ya kupambana." - Emanuel Bwire, mwalimu mkuu msaidizi Tegeta.

2.4.4. Watoto wangapi walipata vyeti?

Mwaka 2012 wanaharakati wa ATD waliwawezesha wazazi wa watoto zaidi 260 maskini kabisa kupata vyeti vya kuzaliwa. Wanaharakati Shabani na Venance walisaidia kusajili baadhi ya watoto

2.5. Watu wazima maskini wanajifunza kusoma na kuandika

2.5.1. Nini maana ya kupata elimu kuditia ATD?

Kujiona siyo bora kunawafanya watu kuwa sugu kwa matukio yanayo vuruga haki. Wanaharakati kuto kujua kusoma na kuandika ni bahati mbaya sana katika kila nyanja ya maisha. Marafiki wanaeleza kuwa elimu inawasaidia watu kujua mambo mengi ya msingi kama vile kutia saini, kuelewa muelekeo wa gari la abiria, kusoma gazeti vitabu n.k. Ni hatua ya kuushinda umaskini uliokithiri na kutengwa.



"Bila ya elimu huwezi hata kuandika jina lako, hivyo elimu ni kitu muhimu sana. Ukiwa na elimu unajenga kujiamini, unaweza kukutana na watu wa tabaka zotena unaweza kongea vizuri. Pia ni rahisi kufanya kazi na hata kusafiri." - Mohamed Selemani, Soko la samaki Magogoni (Mpaa samaki).

"Nadhani vita ya kufuta ujinga ni mapambano dhidi ya umaskini uliokithiri. Baada ya kujua kusoma na kuandika, watu wanafanya mambo ambayo hapo awali walikuwa hawawezi kuyafanya. Ukijua kusoma na kuandika ni rahisi kupata kipato." - Mwalimu Fredrick na mchungaji Tegeta.



2.5.2. Kwa nini baadhi ya watu wazima hawajui kusoma na kuandika?

Hapa Tanzania asilimia 27 ya watu wazima hawajui kusoma wala kuandika kiswahili. Watu wengi maskini hawakupata fursa ya kwenda hata shule ya msingi. Wanalazimika kufanya kazi zisizokuwa za ujuzi ili wapate fedha kwa ajili ya kutunza familia zao. Kutokana na juhudi za kupata fedha kwa ajili ya familia zao inakuwa vigumu kwao kupata muda na ari ya kujifunza.



"Wale ambao sasa wanajifunza kusoma na kuandika, wanaona ingekuwa vema kama wangefanya hivyo walipokuwa watoto, lakini familia zao hazikuwapa fursa hiyo, siyo mkosa yao ni ukweli." - Mama Zulfa muuza kuni la samaki.

2.5.3. ATD inawasaidiaje kujua kusoma na kuandika?

ATD inaendesha kisomo kwa watu wazima ambao wanajifunza kusoma na kuandika kiswahili. Darasa lina wanafunzi wasiozidi 12 nao wanahitimba baada ya miezi 6. Kuna vipindi viwili vyatya muda wa saa mbili, kwa siku mbili kwa juma. Kila mwanafunzi anasaidiwa na rafiki yake kutoka eneo husika ambaye humsaidia na kumpa moyo.

2.5.4. Ni watu wangapi walijifunza kusoma na kuandika?

Mwaka 2012 madarasa yaliendeshwa huko Tandale na Kunduchi. Watu wazima 11 walifafulu bada ya kusoma kwa muda wa miezi sita..

"Nilikuwa hata sijui kuandika jina langu. Wakati nilipoalikwa katika kikao cha ndugu au marafiki, mara zote nilipaswa kuandika jina langu kwenye kitabu, nilikuwa sijui na illibidi mtu aniandikie. Pia nilikuwa sijui kusoma daladala wapi zinapoelekea na ilinibidi kumsubiri konda kutangaza. Ndio maana nilihamasika sana kujifunza.



Ndugu zangu walijivunia sana walipoona najifunza kusoma na kuandika, haswa mume na watoto wangu. Ilikuwa ni muhimu kunitia moyo. Pia mume wangu alijifunza katika darasa hilo hilo. Mwanzoni mwa darasa baadhi ya wanafunzi walikuwa wanaona aibu. Huenda, kwasababu walikuwa hawajui chochote kama mimi. Haraka mno aibu yao ilitoweka ambapo wamejifunza silabu na kugundua kuwa walikuwa wanauwezo wa kujifunza. Mwanzoni wanafunzi wote walikuwa wanahudhuria vizuri na kuwasili mapema ili kujipa mazoezi kwa pamoja. Ndoto yangu ni kujua kusoma gazeti." -Bi Agnes mvunja mawe machimbo ya kokoto Kunduchi.





Mwelekeo kwa mwaka 2013.

Mwaka 2013 tutaendelea kufanya kazi katika vipaumbele vyetu vinne, kuzingatia yafuatayo:

Kipaumbele cha kwanza “kuwasaidia wanachama wa ATD katika maendeleo ya ATD Dunia ya Nne hapa Tanzania” tutafanya:

- Kuwahamasisha na kuwasaidia wanachama wa ATD kwa majukumu mbali mbali ya kujenga harakati hapa Tanzania.
- Kuwasaidia marafiki vijana wa ATD kujadili mambo yao na kuwakaribisha wengine kujiunga na kundi,
- Kuendelea kuboresha na kuongeza nguvu katika ushiriki wa wanachama wa kundi la washauri,
- Kuboresha mawasiliano na kulinda mawasiliano na marafiki wa ATD wanaoishi nje ya Dar es Salaam.

Kipaumbele cha pili “kusaidia, kupitia shughuli na miradi yetu, watu wasiothaminiwa katika changamoto wanazozipata” tutafanya yafuatayo:

- Kutunza mawasiliano na watu wanaofanya kazi katika nzazi za mamlaka, haswa wale wote wanaofanya kazi karibu na maskini watoa huduma kulingana na shughuli zetu,
- Kuwasaidia watu maskini kupambana na changamoto tofauti ili kupata haki zao za msingi,
- Kuendelea kuwasaidia watu maskini kuendesha shughuli kama vile kujifunza kusoma na kuandika, uandikishaji vyeti vya kuzaliwa n.k.

Kipaumbele cha tatu “kuunda uhusiano kikanda na dunia”:

- Tutashiriki katika mchakato wa mipango, ikiwemo na kikao cha kimataifa cha kubadilishana mawazo na timu zilizo mbali,
- Tutahakikisha kuwepo wa kiswahili katika tovuti tofauti za harakati,
- Tutawakaribisha wawakilishi kutoka timu nyinge za ATD,
- Tutaendelea na mafunzo kuwaruhusu wanachama wa ATD Tanzania kuwakilisha na kujenga harakati ndani na nje ya nchi yao.

Kipaumbele cha nne: Kuzingatia ujenzi wa ATD hapa Tanzania. Tutafanya yafuatayo:

- Tutaendelea kuchangisha fedhaza kuendesha miradi yetu ndani ya Tanzania ili kukidhi mahitaji ya gharama zote.
- Kuendeleza uhusiano wetu mzuri na wafadhili ambao tumeujenga kwa muda mrefu na pia kutafuta njia nyingine za mapato kwa ajili ya miradi yetu.
- Kuendelea na mlolongo wa kulinda nyaraka zote za kiwanja cha ATD Mwananyamala.
- Kufanya kazi na kuimarishe timu ya vijana wa Tanzania wanaojifunza ambao husaidia shughuli za timu. Pia watakuwa na nafasi ya kujitolea kwa ajili ya nchi yao na kufaidika kwa kujifunza.

Viambatanisho

4.1. Taarifa ya fedha

- Bajeti ya ATD Dunia ya Nne ina sehemu mbili: Gharama zinazowiana na wanaharakati wa kimataifa wa kujitolea waliopo hapa Tanzania pamoja na posho, michango ya jamii, usafiri n.k.
- Gharama zilizotumika na ATD Dunia ya Nne Tanzania ni kama ilivyo ainishwa hapa

	2011		2012	
	Euro	Euro		Shilingi kitanzania
Matumizi				
1, Gharama za ofisi	5,251		5,042	10,285,680
Maji	48	49		99,960
Umembe	82	138		281,520
Vifaa vidogo vidogo	510	41		83,640
Kodi na uchakavu	3,463	3,463		7,064,520
Nyingine	94	86		175,440
Mshahara w a mlinzi	1,054	1,265		2,580,600
2, Huduma za kiofisi	3,419		2,632	5,369,280
Gharama ndogo ndogo	513	80		163,200
Vifaa vya ofisi	541	741		1,511,640
Ukaribisho	584	675		1,377,000
Vitabu na magazeti	195	275		561,000
Ada na kodi (kiw anja)	904	228		465,120
Stempu	344	363		740,520
Simu na mtandao	338	270		550,800
3, Usafiri	3,349		3,196	6,519,840
Ndani ya nchi	253	0		0
Mafuta/petroli	386	386		787,440
Matengenezo/uchakavu	553	883		1,801,320
Kodi/bima ya pikipiki	30	12		24,480
Usafiri nje ya nchi	1,050	1,620		3,304,800
Viza na bima ya safari	1,077	295		601,800
4, Shughuli	7,235		17,254	35,198,160
Usafiri ndani ya nchi	284	906		1,848,240
Fedha ya kujikumu/familia	164	72		146,880
Mafunzo kw a vijana	3,088	2,610		5,324,400
Chakula	147	737		1,503,480
Matumizi kw a shughuli	3,398	11,029		22,499,160
17.	154	420		856,800
Pesa iliyobakia		1,480		3,019,200
5, Timu, wanafunzi	17,855		7,240	14,769,600
Mishahara	2,179	5,470		11,158,800
Michango/hifadhi ya jamii	436	1,094		2,231,760
Mafunzo ya lugha	960	676		1,379,040
Michango kw enda kw a jeshi la w anaojitolea	14,280	0		0
6, Gharama za benki	121		149	303,960
Huduma za benki	121	149		303,960
Jumla ya Matumizi	37,230		35,513	72,446,520
Mapato				
Kuuza vitabu	101	26		53,040
Misaada na michango	37,084	33238		67,805,520
Michango toka Ufaransa	45	0		
kimataifa		2249		4,587,960
Jumla ya Mapato	37,230		35,513	72,446,520

4.2. Kwa taarifa zaidi

Kitaifa na Kimataifa wasiliana nasi kwa:

Makao Makuu ya Shirika Kimataifa

Paris : ATD Fourth World

12, rue Pasteur
95480 Pierrelaye, France
tel : (33) 1 30 36 22 11 / fax : (33) 1 30 36 22 21

New York : Fourth World Movement

172 First Avenue
New York, NY 10009-4508, USA
tel : (1) 212-228-1339 / fax : (1) 212-777-6491

Geneva : Maison Joseph Wresinski

Chemin Galiffe, 5
01201 Geneva, Switzerland
tel : (41) 22 344 41 15 / fax : (41) 22 344 47 77

Dar es Salaam, Tanzania

ATD Dunia ya Nne

Mwananyamala A (Igusule street, n°34)
P.O. Box 61786 Dar es Salaam
E-mail : atd.tanzania@gmail.com

Mitandao: Kimataifa,, 17 Oktoba, Tanzania...

ATD Dunia ya Nne Harakati za Kimataifa - mtandao wa kiingereza:

www.atd-fourthworld.org

Siku ya Kuutokomeza Umaskini Uliokithiri Duniani - mtandao wa kiingereza

www.overcomingpoverty.org

ATD Dunia ya Nne - ukurasa wa mitandao na nyaraka za marejeo...

kiingereza: www.atd-fourthworld.org/-Tanzania_549-.html

kiswahili: www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html

Joseph Wresinski, mwanilishi wa ATD Dunia ya Nne -mitandao:

kiingereza: www.joseph-wresinski.org/Father-Joseph-Wresinski.html

kiswahili: www.joseph-wresinski.org/Unaye-mama-wewe.html